# W a k r i s t o   h o d a r i

Hadithi za watakatifu zilizotwaliwa katika kitabu "Wahre Gottsucher" kilichotungwa na P.Bihlmeyer O.S.B. na kufasiriwa na P.Beatus Iten O.S.B.

---

Kimepigwa chapa

Imprimatur:

Peramiho, den 21. Juni 1939

+ Gallus Steiger O.S.B.

Abt-Bischof

Yaliyomo

Mazedonyo mtakatifu mweremiti uk.
Saturnini mtakatifu na Wakristo wake, mashahidi .....
Karapi mtakatifu Askofu, na Papili mtakatifu, Mashemasi, mashahidi ..................
Yuliana mtakatifu ....................
Epulyo mtakatifu mshemasi na shahidi ..............
Teresia mtakatifu wa Mtoto Yesu ....................
Gerardi mtakatifu ..................................
Antonio mtakatifu Baldinuchi .......................
Franz Ksaver mtakatifu mtume wa Uhindi na Japani .....
Melania mtakatifu ..................................

M a z e d o n y o mtakatifu mweremiti

24. January 450.

## WATAFUTAJE?

Palikuwa na mtu mmoja, jina lake Mazedonyo, aliyeishi peke yake. Kazi yake kusali na kutubu. Kwanza alishinda miaka 45 mchana na usiku katika shimo refu. Baadaye alikaa mwituni.

Siku moja Bwana Nyama alifika mahali pale naye alikuwa akiwinda. Hapo akamkuta mweremiti huyu. Akashangaa akamwita akisema:

"Bwana wangu, niambie wafanya nini hapa? Watafuta nini katika mwitu huu?"

Mweremiti akasema: "Basi, nitakueleza, lakini tafadhali niambie kwanza wewe watakaje hapa?"

Mwindaji akichekelea akajibu: "Lo! Nawinda wanyama kama ngiri na mbawala na mbundju na wengineo."

Akanena mweremiti: "Nami namtafuta Mungu wangu. Siwezi kuacha mawindo hayo bora mpaka nimwone Mwenyewe uso kwa uso."

Bwana Nyama akanyamaza, na baadaye akaondoka akiyawazia sana maneno aliyosikia.

Mazedoyo mtakatifu aliishi wakati wa mwaka 400 tangu kuzaliwa Bwana wetu Yesu Kristu. Kumbe hata sasa watu hufanya kama zamani zile. Wengine huwinda anasa, na wengine humtafuta Mungu.

Nawe msomaji watafutaje?

S a t u r n i n i mtakatifu, Padre, na Wakristo wake, mashahidi.

11. Februari, 303, Karthago

Misa takatifu ya Dominika

Zamani za Kaisari Dioklesian wakristo walidhulumiwa vikali sana. Siku ya Dominika, walipokuwa wakihudhuria misa takatifu, wakristo 49, wanaume na wanawake na watoto pia, walishambuliwa na wapelelezi wa Kaisari, wakatiwa minyororo na kupelekwa gerezani ~~mwa~~ Karthago.

Bwana shauri alimwuliza Padre Saturnini kwa ukali: "Ndiwe aliyewakusanya hawa kwa ibada iliyokatazwa na Kaisari?"

Padre akajibu: "Ndimi, bwana, tulikuwa tukisali."

Bwana shauri: "Kwa sababu gani mmevunja amri ya Serikali?"

Saturnini: "Hatuwezi kuacha misa takatifu siku ya Dominika, maana ni amri ya Mungu."

Kwa sababu ya majibu hayo padre aliteswa akapigwa majeraha mwilini mwake. Lakini Saturnini alimwamini Bwana Yesu Kristo kwa uthabiti. Wakati wote alipokuwa akiteswa alidumu kuomba hivi: "Ee Bwana wetu Yesu Kristo nakusihi, unihurumie! Mwana wa Mungu unisaidie. Nimefuata sheria yako tu ya kukutolea sadaka ya misa takatifu." Hayo ndiyo maneno yake ya mwisho ya Padre huyu mzee, Saturnini mtakatifu.

Kabla Saturnini hajazimia roho, mkristo mwingine jina lake Emeritus, alisimama akaenda mbele ya wakuu akasema kwa sauti kuu: "Mimi ndimi niliyewakosesha hawa wote. Maana nyumbani kwangu ndiko walikokusanyika." Mwamuzi alimhoji: "Kwa sababu gani uliwakubalia hayo?" Majibu yake Emeritus ni: "Kwa kuwa hao wote ni ndugu zangu, wala siwezi kuwakataza." Mwamuzi alisema: "~~Mbona~~ Kwa nini imekupasa kuwazuia wasikusanyike nyumbani mwako." Emeritus akasema: "La, sina ruhusa kuwazuia, kwa kuwa sisi wakristo ~~hatuw~~ hatuwezi kuishi pasipo kusikiliza misa takatifu siku ya Dominika." Naye pia wakati wote alipoteswa vikali mno alidumu kusali, akafa shahidi wa dini.

Wala wenzake wengine wote hawakuhurumiwa. Tena na tena walisema: "Sisi wakristo, hatuwezi kutenda namna nyingine. Lazima tuishike sheria takatifu ya Mungu, hata tukihukumiwa kuuawa."

Nguvu ile ya siri, isiyoshindikana, ndiyo baraka ya misa takatifu ya Dominika. Ilikuwa imara ya mwili na ya roho kwa mashahidi wale. Iliwatia nguvu kuifuata amri ya Mungu kwa uaminifu.

Mwisho aliitwa Hilariani, naye bado mtoto. Hata yeye hakukubali kuiasi dini yake, ijapokuwa alitishwa na kubembelezwa kwa kila namna. Alijua neno moja tu: "Fanya utakalo, mimi mkristo." Akateswa hata akafa, na maneno yake ya mwisho ni: "Deo gratias, namshukuru Mungu kwa neema hii ya kutoa damu yangu kwa ajili yake."

K a r a p i mtakatifu, Askofu na Papili mtakatifu Mshemasi, mashahidi

---

13. Aprili 116

## Tuvumulie kwa furaha!

"Mimi mkristo! Namwabudu Yesu Kristu, mwana wa Mungu. Wazima hawatolei sadaka kwa miungu isiyo na uzima." Ndivyo alivyosema Karapi askofu mbele ya mwamuzi. Naye Papili alisema vile vile : "Hata mimi mkristo, halipatikani jambo kubwa na zuri zaidi."

Kwa sababu ya maneno hayo waliraruliwa na makucha ya chuma. Karapi aliendelea kusema: "Mimi mkristo," mpaka aliposhindwa kusema neno. Lakini Papili alinyamaa kimya.

Mwamuzi alipoona kuwa hawezi kitu, aliamuru wachomwe moto wote wawili, bado wa hai. Lakini mashahidi hao waliposikia hukumu hiyo walifurahi sana. Wakafuliza mwendo wao ili wafike upesi katika Amfiteatro ndilo jumba walipoteswa mashahidi wa dini na ugeni wao uishe duniani wafike kwao mbinguni.

Kwanza Papili alifungwa katika mti kwa misomari, Baadaye waliweka kuni karibu na kuzitia moto wakasikia Papili akadumu kusali hata kuzimia roho.

Karapi alipofungwa katika mti, alichekelea. Waliokuwapo wakamwuliza: "Unacheka nini?" Mshahidi akajibu: "Nimeona utukufu wa Mungu, basi, nafurahi."

Akamwambia askari yule aliyewasha moto: "Sisi sote tunayo asili moja kutoka mama mmoja, ndiye Eva. Nasi tunao mwili wa namna moja tu. Sababu hii, basi, kufa kwa moto kunaleta maumivu kweli kweli. Lakini tukikumbuka hukumu ya mwisho twaweza kuvumilia hayo yote kwa furaha." Halafu akainua macho juu uwinguni akaomba: "Atukuzwe Bwana Yesu Kristu, Mwana wa Mungu,aliyenihurumia mimi mkosefu, na kunipokea kwake." Baada ya maneno hayo akafariki.

Wanapatikana hata leo watu wenye kucheka na kufurahi pamoja katika taabu na mateso? Hakika wako. Ndio watu wa imani wajuao mavuno ni tuzo ya taabu ya kazi.

Y u l i a n a mtakatifu

19. June 1341.

Muhuri wa hostia takatifu

Yuliana yu karibu kufa. Lakini alikuwa bado na ~~haja,~~ shauku ~~maana alitaka~~ kumpokea Mungu na Mkombozi wake katika umbo la mkate kwa masurufu. Kumbe ugonjwa mbaya sana wa tumbo ukamzuia. Hata padre, mtu mwenye huruma ya kimungu, alishindwa kutimiliza maombi yake ya mwisho. Yuliana ole wako!

Mara macho yake yalimulika . Kwa shida alimwambia padre maneno kidogo. Naye aliondoka akarudi upesi akichukua Ekaristi takatifu katika chombo cha dhahabu. Lo! Uso wa mgonjwa uling'ara kama jua kwa heri yake kuu.

Padre alitandika nguo nyeupe kabisa kifuani mwake bikira huyo safi akaweka juu yake kwa ibada kuu Ekaristi takatifu. Lo! Mkate wa mbingu, ndicho chakula cha malaika , ulipogusa kifua cha bikira ukawa ulififia kama kuliwa na macheche ya moto mbele ya watu waliohudhuria.

Yuliana alifumbua tena mara moja macho yake yenye kujaa ~~na~~ heri kubwa mno. Baadaye moyo wake ukavunjika kwa tamaa na furaha ya kumwona Yesu Kristo mbinguni.

Walipoosha maiti na kutia sandani ilionekana alama ya ajabu kama muhuri mahali pale pale pa moyo wake, ilipolalia Ekaristi takatifu. Ilifanana na hostia. Sura ya Yesu Kristo msalabani ilidhihirika vizuri sana.

Tangu zamani haikusikilizwa habari ya ajabu namna hii. Je, Mkristo wee, roho yako haipewi neema ya namna hii? Yesu, unayempokea katika komunio takatifu, ataka ufanane naye. Au haikusafishii roho yako na kuifanya nyeupe na safi kama hostia? Haikugeuzi wewe kuwa mpole na mwema kwa wenzako? Hakika hata wewe ukipenda kujitolea sadaka kwa Mungu, utafanana na Yesu msulibiwa.

## E p u l i o mtakatifu, mshamasi na shahidi

21 Agosti 304

### Maneno na uzima wa milele

Epulio alisimama barazani mbele ya Bwana mkubwa, naye alikuwa na kitabu kitakatifu mikononi mwake: "Kitabu hiki umekileta wewe hapa?" "Ndiyo, Bwana mkubwa, unavyoona. Nalikamatwa mwenye kitabu hiki."

"Soma ndani yake!"

Epulio alifungua kitabu akasoma: "Heri watu wanaosubuliwa kwa ajili ya mambo mema kwa kuwa ufalme wa mbinguni ni mali yao." Tena pengine: "Ikiwa mtu anataka kunifuata, basi ajitwike msalaba wake anifuate."

Alipokwisha somewa maneno hayo na mengineyo Bwana mkubwa akamwuliza: " hii ni nini?"

Epulio akanena: "Ndiyo sheria ya Bwana wangu niliyopewa naye."

"Na nani?"

"Na Yesu Kristu, Mwana wa Mungu wa kweli." Bila hofu alifanya ishara ya msalaba akisema: "Nimekwisha kukuambia hata nakuambia tena mimi mkristo na nimezoea kuyasoma maandiko matakatifu."

Bwana mkubwa : "Sababu gani ulificha kitabu hiki kilichokatazwa na kaisari? Sababu gani hukukitoa?"

Epulio: "Sababu mimi mkristo wala sina ruhusa kukitoa. ~~Mbona~~ ndani yake umo uzima wa milele. Anayekitoa apoteza uzima wa milele. Siwezi kukitoa kitabu hiki, nisije nikapoteza uzima wa milele."

Basi akateswa tena vikali mno. Wakati wote akadumu kusali mpaka nguvu zote za mwili zilipomwacha. Alipopata tena nafuu kidogo alifungiwa kitabu hiki shingoni mwake akapelekwa kuuawa.

Mpiga mbiu alitangulia na kutangaza: "Epulio ni mkristo na adui wa miungu na wa Kaisari." Epulio hodari wa kuvumilia alisema mara kwa mara: "Ee Mkombozi wangu, Mungu wangu, asante sana, asante sana."

Alikubali kutoa damu yake lakini hakuweza kutoa kitabu kitakatifu.

Siku hizi si lazima kuficha kitabu kitakatifu wala hakuna hatari ya kuteswa kwa ajili yake. Je, wakristo wangapi wanacho? ~~Mbona~~ kitabu kitakatifu ndicho kitabu cha Mungu, ni bora kuliko vitabu vyote.

"Ee Bwana, tumwendee nani? Wewe unayo maneno ya uzima wa milele!"
(Yoh. 6.69.)

T e r e s i a mtakatifu wa Mtoto Yesu

30 Sept. 1897.

Upendo waweza yote.

Nataka kuwasomesha neno moja tu lililo katika habari zake mtakatifu Teresia Mdogo. Yeye mwenyewe asimulia: "Palikuwa mtawa mmoja mwenzangu naye mwema kweli, lakini hakunipendeza kabisa. Hata lo lote alilotenda lilinichukiza tu. Nadhani ndiyo hila ya shetani kunionyesha tabia zile tu zilizonichokoza; lakini nalitaka kutumia mambo hayo ili nishinde tabia yangu mbaya , nikatimilie amri ya kupendana, si moyoni tu ila hata kwa matendo yangu. Basi nilifanya bidii kuwa na mapendeleo na machekeleo kwa mtawa huyu kama angalikuwa rafiki yangu mpenzi mno. Kila nilipokutana naye nilimwombea kidogo moyoni mwangu nikamtolea Mungu fadhali zake za siri, na vile nilifahamu namfurahisha Mkombozi wangu, kwa kuwa kila mstadi hufurahi kusifiwa kazi yake. Mungu pia aliyeumba roho za watu kwa ustadi mkuu hupendezwa tusipoangalia makosa madogo tu ya nje ya mwenzetu, hufurahi tukiangalia uzuri na fadhali ndani ya moyo, ndiyo hekalu anamokaa Mungu.

Sikutosheka kumwombea yeye aliye chemchemi ya mashindano mengi rohoni mwangu. Nikatafuta nafasi yo yote tena kwa kumfurahisha kwa kila namna ya mapendo. Ikiwa nalishikwa na kishaushi kumjibu kwa ukali, nalijishinda nikamjibu kwa upole, au nikaanza kuongea juu ya mashauri mengine. Lakini mara nyingi adui mbaya shetani aliponishambulia mno nilimtorokea mwenzangu yule asione mashindano moyoni mwangu.

Loo! Siku moja mtawa yule aliniuliza kwa uso wa kung'aa: "Teresia, mpenzi wangu, ningefurahi sana kusikia kwa sababu unanichekelea kwa mapendeleo kila tunapokutana." - Hakufahamu ya kuwa ndiye Yesu aliyetia upendo wake moyoni mwangu , maana nalimjua Yesu anakaa moyoni mwake ndiye mkombozi wangu mwenye kugeuza mambo magumu kuwa matamu."

G e r a r d i  mtakatifu

12 Okt. 1155.

Ufunguo uliopotea.

Gerardi aliyekuwa mtumishi wa askofu wa Lasedonya alisimama sokoni mbele ya kisima akatazamia ndani kwa kituko. Ufunguo wa nyumba ulimchopoka. Ah! hahati mbaya - ufunguo umo ndani ya kisima chini kabisa. Haikosi bwana akirudi nyumbani na kushindwa kuingia atafanya matata sana sana. Kumbe! akili haikumpotea mtumishi huyu mwema. Alipiga mbio akachukua katika kanisa lililo karibu sanamu ya mtoto Yesu. Watu wengi walikusanyika pa kisima wakipekua kuona yatapataje.

Gerardi akambembea mtoto Yesu akimwambia: "Ee katoto Yesu, ee Yesu mpenzi wangu! Ndiwe peke yako uwezaye kunisaidia katika shida yangu. Juu yako kunirudishia ufunguo."

Basi akafunga sanamu ya mtoto Yesu kwa kamba akaishusha ndani ya kisima. Akaomba tena:"Katoto Yesu, katoto mpenzi, unirudishie ufunguo."

Pole pole alivuta kamba juu. Mara watu wote wakalia kwa mshangao, kwa kuwa sanamu ya mtoto Yesu iko juu, nayo imeushika ufunguo mikononi mwake.

Gerardi aliupokea kwa furaha na shukrani akapeleka tena sanamu ya mtoto Yesu kanisani.

Sisi sote tulikuwa tumepotea ufunguo wa mbinguni. Ulianguka shimoni. Watu wote walipigwa na bumbuasi wasijue la kufanya. Hayuko wa kuwasaidia.

Hatimaye akaja Mwana wa Mungu "ndiye mtakatifu na mwenye ukweli anayechukua ufunguo wa Daudi naye akifungua hakuna awezaye kufunga, na akifunga hakuna awezaye kufungua."(Ufunulio 3,7). Yesu Kristu alitufungulia tena mlango wa uwingu

A n t o n i o mtakatifu Baldinuchi

6. Nov. 1717.

Kama majani ....

Siku moja Antonio mtakatifu alikuwa akihubiri shambani mbele ya watu wengi. Mara alipaza sauti akinena: "Watoto wangu, mwataka kujua jinsi siku kwa siku roho za wakosefu zinavyoanguka motoni? Tazameni watu wabaya huanguka motoni sawa sawa na majani ya mwembe huu."

Mara majani ya matawi yakapukuswa. Ukasikilika mchakachochakacho kama wa makundi mengi ya nzige. Nayo mvua ya majani ilikuwa kwa wingi sana hata mtu hawezi kumwona jirani wake. Mambo hayo ya kitisho yalionekana muda wa kusali "Baba Yetu" mara tano. Watu wote walipatwa na hofu wakapiga magoti wakalialia: "Huruma, huruma!"

Hatibu akasema: "Basi! Yatosha!" na ~~sasa hivi~~ mara moja mvua ya majani ilikwisha. Mwembe huu ulionekana unayo majani machache tu katikati ya miembe mingine yenye majani tele.

Ndivyo wanavyopotea wakosefu. Bali watu wema, mbali kabisa. "Mtu mwema ni kama mti uliopandwa kando ya mto mwenye maji mengi. Mti huo huzaa matunda kwa wakati wake, na majani yake hayapukutiki. Nayo yote atendayo atafanikiwa." Zaburi 1.

"Utimizeni wokovu wenu kwa kuogopa na kutetemeka." Phil. 2,12.

27. Nov. 1552.

## Mwanga na giza

"Bwana nipe roho za watu!" Hiyo ndiyo sala aliyopenda Franz Ksaver mtakatifu. "Bwana nipe roho za watu!" Hiyo ndiyo nia yake alipotoka Ulaya na alipoabiri katika merikebu ya bidhaa miezi mingi kwa taabu kubwa kabisa akizunguka bara nzima ya Afrika. "Bwana nipe roho za watu!" Hiyo ndiyo aliyotaka alipowafundishafundisha Wajapani.

Sifa zake zilizidi siku kwa siku. Mfalme mwenyewe alimkaribisha nyumbani mwake. Kwa sababu hii makuhani wa kipagani walimchukia. Walifanya hila ili kumaliza kazi ya misionari huyu kwa mara moja: yaani walimtaka abishanie dini pamoja na walimu wao.

Mfalme aliyempenda huyu mtu wa Mungu alimwogopea. Lakini yeye alipoona mashaka ya mfalme alimsihi awaite walimu naye apate ruhusa ya kujadiliana nao. Franz mtakatifu alinena: "Ewe mfalme mkuu, usinihofie. Kwa sababu ninayoeleza si elimu ya kibinadamu iliyofundishwa katika mashule makubwa wala si uzushi wa akili tu. La! Dini ninayohubiri ni mafundisho yaliyotoka mbinguni , asili na mwalimu wake Mungu mwenyewe. Walimu wote wa Japan na walimu wote pia wa dunia hawawezi kuishinda , kama giza ya usiku haimalizi mwangaza wa jua.

Basi walibishana. Franz Ksaver aliwashinda walimu wa kipagani.

"Neno langu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima ya kibinadamu. Nayo imani yetu ni neema ya Mungu mwenye kutupenda na kuturumia." Ndiyo maneno aliyokwisha sema mtakatifu Pauli zamani za miaka 1900 iliyopita. Na maneno hayo yatakuwa na nguvu hata mwisho wa dunia. Mashindano ya mwanga na giza hayatakwisha nayo matumaini ya wakristo na furaha yao ya kushinda hayatakwisha.

M e l a n i a  mtakatifu

31. Des. 439 Yerusalemuni

Njia nyembamba

"Naye aliposikia haya akasononeka kwa kuwa alikuwa na mali nyingi mno." Lukas mtakatifu mwinjilisti aliandika habari hiyo ya kijana mtajiri.

Piniani na Melania bibi yake, watu wema na wacha Mungu, waliishi katika mji wa Roma. Nao walikuwa wamerithi mali ya shilingi milioni na milioni.

Siku moja waliota ndoto kama walilazimishwa kupenya ufa mwembamba mno wa ukuta. Waliona taabu sana hata kushikwa na hofu ya kuzimia roho.

Asubuhi yake Melania alimwambia mumewe: "Mali ya dunia ni mzigo mzito sana . Hatuwezi kuuchukua. Afadhali kuiacha mali yetu upesi na kujitwika nira nyepesi ya Yesu Kristo."

Piniani akakubali shauri la bibi kama shauri la Mungu mwenyewe. Basi waliwagawanyia ~~wa~~fukara na maskini mali yao kwa ukarimu.

Kwa kuwa walifiwa na watoto wao wawili walipokuwa bado wachanga walikusudia mahali pao kutunza na kusaidia wagonjwa mjini mwao. Waliwapokea wageni nyumbani mwao wakawapa zawadi tele. Kwa ~~wa~~fukara na maskini walikuwa na mkono wa utoaji ~~mrefu~~. Tena huenda kutuliza wafungwao gerezani. Kila mwenye uchungu na shida huwatumainia wao. Waliyeyusha vyombo vyao vya dhahabu na fedha ili kufulisha ~~tengeneza~~ vyombo vya kanisa. Huwanunulia watawa wanaume na wanawake ~~ma~~nyumba na mashamba ya kuwatosha kukaa ~~katika~~ utawani mwao.

Walipokuwa wamekwisha kugawia yote waliyo nayo walitoka Roma wakahamia Yerusalemu. Ndipo walipokaa katika hospitali ya wageni. Tena walikuwa hawana kitu cho chote. Melania alipougua alikosa hata kitanda na mto yaani sasa ni ~~wa~~fukara kabisa wakitumaini sadaka walizopewa kwa ajili ya Mungu. Kweli walikuwa wametua mzigo wa utajiri na kujitwika mzigo wa ufukara.

Basi Piniani aliingia utawani katika monasterio iliyo juu ya mlima wa mizeituni. Melania alikusanya mabikira akaweka monasterio ya wanawake mjini ~~mwa~~ Yerusalemu. Ndimo alimoishi siku zake zote akiangalia neno moja tu ndilo kupata utakatifu.

Yule kijana mtajiri alihuzunika alipoitwa na Mungu kuacha mali yake yote. Bali Melania! Moyo wake ulijaa furaha kwa kuacha yote na kujitoa mwenyewe kwa Mungu.

"Ingieni mkipita mlango ulio mwembamba. Maana njia iendayo hata ~~kwa~~ upotevu ni pana , na mlango wake mpana, na wengi waingiao kwa mlango huo. Bali njia ni nyembamba iendayo hata uzima, na mlango wake ni mwembamba; nao waionao ni wachache." Mat. 7, 13-14.

# Mtk. Katarina wa Siena

+ 29. 4. 1380.

Naona njaa!

"Wenye heri wanaoona njaa sasa,
kwa kuwa watashiba!" Lc.6,21.

Mtk. Katarina wa Siena hulapa mara kwa mara njaa ya kupokea Komunio takatifu. Kumwona saa zile ungalidhani ana homa kali au anateswa na maumivu makubwa mno. Kumbe kuangalia zaidi , ungalifahamu kama njaa ya kupokea Mungu wake katika Ekaristi takatifu imemchoma.

Siku nyingi kidogo Katarina hakupata nafasi ya kupata chakula cha roho. Siku zile zilikuwa siku za kufunga kweli. Alikuwa na njia moja tu ya kujipatia faraja ndiyo kukaa karibu na Yesu katika Ekaristi takatifu. Yeye mwenyewe alieleza: "Nikishindwa kupokea Ekaristi takatifu , tamaa yangu ya Komunio hutulizwa nikijua Sakramenti takatifu ipo hapa nami naweza kuitazama. Hata mbele ya padre, aliyesoma misa takatifu asubuhi, roho yangu hufarijiwa na kushibishwa."

Baba mtakatifu Gregori XI, alipopata habari hiyo, alimruhusu bikira kuwa na kikanisa nyumbani wake, kusudi Katarina apate kutulizwa kwa kukaa daima karibu na Yesu.

Kila asubuhi tamaa ya Ekaristi takatifu ilipozidi Katarina alimwambia padre: "Baba, naona njaa! Kwa ajili ya Mungu, nipe chakula cha roho! Basi padre yule humtolea misa takatifu na kumshibisha kwa Komunio takatifu. Hapo njaa yake hugeuka kuwa heri kuu.

Hiyo ndiyo neema kubwa aliyotoa Papa kwa bikira wa Siena. Kwani wakati ule ilikuwa vigumu kukaribia meza ya Mungu. Siku hizi tunayo bahati njema. ~~Mbona~~ Kwa nini Papa ametualika karamu takatifu kila siku.

Nawe pia waona njaa? Wapokea kila unapopata nafasi? Wafanya tamaa ya kujiunganisha na Yesu? Wamchungulia ukipita kanisa?

## Mtakatifu L u s i a  F r e i t a s , mjane na mshahidi

+ 10. 2. 1622 karibu na Nagasaki

Diego usitoroke!

Lusia mzaliwa wa Ujapani, alikuwa mkristo tangu utoto wake. Baada ya kufiwa na mume wake, alidumu safi katika hali ya ujane. Siku zile dini ya kikristu ilikatazwa kabisa na Serikali ya Japan. Ikiwa wakristo wali~~tambuliwa~~ sakwa na kukamatwa, waamzi waliwatesa vikali mno, kusudi waasi dini yao.

Lusia alipokuwa mzee sana wa miaka themanini, alikamatwa akapelekwa barazani. Walimshtaki kwamba amewapokea wamisionari nyumbani mwake na kuwaficha. Bila hofu alikubali mambo hayo akaikiri dini yake kwa uhodari. Basi alihukumiwa kuteketeswa ndani ya moto. Pamoja naye wakristo wengine 24 walipata hukumu ile ile.

Aliposikia hukumu yake Lusia alitwaa msalaba mikononi mwake akasema: "Ninapenda sana kufa kwa ajili ya Mungu wangu!" Wakristo hao walipopelekwa mahali pa kuuawa Lusia aliwatangulia wanawake wenzake akiwasalisha litania kwa sauti kubwa. Kila mmoja alifungwa ~~kwa~~ penye nguzo akazungushwa na kuni iliyopangwa hata kifuani. Moto ulianza kuwaka. Wapagani walikuwa tayari kuwashangilia watakaotoroka. Wakristo wenzao waliwatazamia mashahidi kwa hofu na kuwaombea sana, asipotee hata mmoja taji la ushahidi.

Maumivu yakazidi. Kumbe wote walivumilia kwa imara. Mmoja tu, jina lake Diego, alianza kusitasita. Lusia aliona mashaka yake. Kwa huzuni kubwa alimwambia: "Vumilia Diego! Usitoroke! Usituachie! Kupona katika moto huo waweza kujipatia miaka kidogo tu nayo itapita upesi. Lakini baadaye hutaepuka moto wa milele. Diego, kaa imara! Vumilia! ~~Mbona~~ Kwa maana furaha za mbinguni zi karibu."

Halafu mzee mtakatifu aliikumbatia nguzo ~~ya kuwakia~~ inayowaka moto aliyofungiwa. Naye Diego alikaa vile vile, akithibitishwa kwa maneno na mfano wa mwanamke huyu hodari. Akafa pale pale.

Nawe mkristo, katika kishawishi, watakatifu milioni waliofariki dunia wakitoa ushuhuda wao na wakristo wengine wengi sana waliokutangulia na walioko sasa hukusihi wewe hivi hivi: "Usitoroke! Usituachie! Vumilia!"

Wapagani na mashetani wakikushauri neno baya, kama kufuata desturi za kipagani au kuasi dini, usikubali!
~~Mbona~~ Kwa maana umepata sakramenti ya kipaimara, basi shika dini yako kwa uthabiti!

# M o n i k a   m t a k a t i f u, m j a n e

+ Nobemba 387

Mungu si mbali.

Agostini mtakatifu, mwalimu wa dini, ametusimulia habari za mwisho za mama yake, Monika mtakatifu.

"Katika safari yetu kutoka Ulaya kurudi Afrika nchi yetu, tulipumzika mjini ~~mwa~~ Ostia, karibu na Roma. Ndipo tulipozungumza maneno matamu na ya upendo, tukisahau yaliyo nyuma , tukiyachuchumilia yaliyo mbele." Fil. 3,13.

Ee! Mbele yako, ewe Mungu, uliye ukweli, tuliulizana juu ya uzima wa milele wa watakatifu. Tuliwaziawazia maneno yale aliyoandika Paulo mtume mtakatifu: "Mambo, ambayo jicho halikuyaona, wala sikio halikusikia, wala hayakuingia katika moyo wa binadamu, Mungu aliweka tayari kwa wampendao."( Kor. 2,9)

Roho zetu zilijaliwa ~~na~~ moto na upendo wa Mungu wa milele. Juu ya mawazo na maongezi yetu tulionja heri ya mbinguni. Baada ya siku tano mama yangu alishikwa na homa kali. Alipoona majonzi yetu alituambia: "Mtazika mama yenu hapa hapa!" Nalikuwa nimenyamaza kwa kuwa nilitaka kulia machozi. Mdogo wangu alinena: "~~Kwamba~~ heri kufa nyumbani, si ugenini." Mama hakukubali maneno hayo akajibu: "Mzike mwili wangu mahali nitakapokufa. Msifanye majonzi juu ya hayo. Ila neno moja nawasihi: Mnikumbukie kila mtakaposoma misa takatifu altareni kwa Bwana!"

Zamani mama alikwisha kutueleza mara moja kwamba haifai kuangalia na kupenda uzima wa duniani, yafaa tu kufa vema.

Tulipomwuliza kama haoni sikitiko maiti yake kuzikwa mbali na nyumbani alijibu: "Mungu si mbali! Siogopi, siku ya mwisho atajua mahali ninapolala, atanifufua."

Basi mama yangu alifariki dunia siku ya tisa tangu alipopatwa na ugonjwa. Alikuwa na umri wa miaka 56.

Tusikilize na tusomeshe misa takatifu kwa ajili ya marehemu!

## L u d o v i k i mtakatifu, mfalme wa Wafranza

+ 25.8.1270.

Dhambi ya mauti.

Ludoviki alipokuwa bado mtoto matumaini na uchaji na upendo wa Mungu ziliota vizuri sana katika moyo wake. Kwa hiyo mafundisho ya mama yake, ndiye Blanka mtakatifu, yalimfaa sana. Mama huyu aliangalia mwanawe afanye urafiki na vijana wema tu na kila Dominika na sikukuu aende kanisani kusikiliza misa takatifu na neno la Mungu. Ludoviki alikumbuka mafundisho hayo maisha yake yote. Hasa hakusahau neno lile kuu la mama yake kwamba "Ningependa zaidi kusikia kama umekufa kuliko kusikia kama umetenda dhambi ya mauti."

Namna alivyolishika neno hilo tunaona wazi katika habari aliyosimulia msiri wake:

"Siku moja mfalme mtakatifu aliniuliza hadhara ya wageni wengi akisema: "Jemadari, Mungu ni nini?"

Nikamjibu: "Mfalme wangu, Mungu ni roho kamilifu na njema kabisa, hata hakuna roho njema kama yeye."

Mfalme akasema: "Vema! - Basi niambie tena, ungependa zaidi kuwa na ukoma au kuwa na dhambi ya mauti?"

Sikuweza kumwambia uwongo. Basi nilivyowaza moyoni nilimjibu mara: "Ningependa zaidi dhambi za mauti thelathini kuliko kuwa ukoma."

Wageni walipoondoka mfalme alinialika kukaa kitako karibu naye akanena: "Rafiki yangu, ulipataje kujibu vibaya hivi?" Nikamjibu tena: "~~Mbona~~ Kwa nini ninawaza na ninasema hivi hata sasa." Basi mfalme akaniambia: "Mjinga we! Wajidanganya mwenyewe. Hujui kama ukoma wa mwili si mbaya na mchafu kama ukoma wa roho ndiyo dhambi ya mauti? Roho iliyo na dhambi ya mauti inafanana na shetani. Hakuna ukoma mbaya zaidi. Basi nakuomba sana , kwa ajili ya Mungu na kwa ajili yangu mimi uandike maneno haya katika moyo wako. Afadhali kupata ukoma na magonjwa mengineyo na taabu yo yote kuliko kufanya dhambi kubwa moja tu."

Ndivyo hivyo! Kwa kuwa mtu akifa anapotea ukoma wa mwili. Lakini mtu akifa katika hali ya dhambi ya mauti, atakaa katika hali hiyo daima. Ukoma wa roho utaambata naye, hautakwisha milele."

Afadhali kufa kuliko kufanya dhambi ya mauti.

Mtakatifu K o n r a d i , askofu

+ 26.11.975.

Ndege wawili.

Maaskofu wawili, Konradi mtakatifu na rafiki yake Ulariki mtakatifu walikaa pamoja kandoni mwa mto mkubwa, jina lake Reno, ambapo maji yake yanaanguka chini kabisa kwa ngurumu na nguvu nyingi sana. Walipoitazamia tamasha hii ya ajabu, waliona ndege wawili walioruki arukia daima miamba iliyomo mtoni. Ndege walipoanza kuchoka walikamatwa na maji yenye nguvu mno. Walifaulu kutoka , wakazamishwa tena na wakaweza kutoka tena.

Watakatifu hawa mara walijulishwa rohoni mwao kama mchezo huu mbaya ni mfano. Walifahamu ndege hawa wawili ni mfano wa roho za marehemu toharani. Hujaribu kuruka juu, kumbe hawawezi bado kwa sababu hawajasafishwa kabisa.

Basi maaskofu walikusudia kuwasaidia marehemu. Mtakatifu Ulariki, aliyekuwa mgeni wa mwenzake, alitangulia kutolea sadaka ya Yesu Kristu. Mungu aliipokea kwa huruma. Mara alionekana ndege mmoja tu katika shida zake. Ndipo naye mtakatifu Konradi alisoma misa takatifu na mara hata ndege ya pili alikombolewa akapata kuruka juu mbinguni.

Kweli wako watu wa namna mbili wanaohitaji msaada wetu . Wanahangaikahangaika. Wanaomba tuwasaidie.

Duniani hapa watu wengi hujaribiwa mno wakikamatwa na maji ya shauku na tamaa mbaya. Kwa hiyo wanakaa daima katika hatari ya kupotea. Wanaanza kuchoka katika mashindano yao wakianguka na kusimama, kuanguka na kusimama. Watu wenye vishawishi vingi huchoka. Haitoshi kuwashauri na kuwafundisha tu. Lazima kuwaletea shime.

Nao wengine wanaotaka msaada ndio maskini katika mateso ya toharani Wanashindwa kwa nguvu zao kutoka katika maji mabaya ya mateso yao. Basi, tuwasaidie kwa misa takatifu na kwa kuwapatia rehema.

Wa heri wanaohurumia wakosefu na maskini. Siku ya maamzi, ndiyo siku ya hasira, Mungu atawahurumia wao pia, kwa kuwa waliofanya huruma nao pia watapata huruma.

# Mtakatifu M a r i a  S a l e s i a

\+ 7.10.1875.

Enendeni wakati mlipo na mwanga! (Yoh. 12,35.)

Maria Salesia alipokuwa bado mtoto alifuatana na ~~mamake~~ mama yake kumwangalia rafiki yake. Mwanamke huyu mgonjwa sana alilialia akisema kwa uchungu ~~mkubwa~~ mwingi: "Ee Mungu, Hasara, hasara! Kuona mwanga wakati nguvu zilipokwisha!"

Mwana hakufahamu maana ya maneno haya. Lakini hakuweza ku~~zi~~sahau uchungu, ~~na~~ kilio na ulalamizi wa mgonjwa.

Wakati waliporudi nyumbani Maria Salesia aliuliza akisema: "Mama! Mgonjwa alinenaje juu ya mwanga?"

Mama akajibu: "Mwanamke huyu alikuwa mkristo mwema, lakini sasa katika saa ya kufa Mungu alimjulisha kwamba angaliweza kufanya bidii zaidi katika dini. Naye anaona uchungu kwa kuwa hakufahamu neno hili tangu zamani."

Tangu siku ile Salesia husali mara nyingi: "Mungu wangu mpenzi, nakusihi, uniangazie wakati ninapoweza bado kujikamilisha!"

Mungu alisikiliza sala zake akampa mwanga tele njiani kwa yeye na kwa wengi wengine aliowaongoza utawani. Hivyo hakutembea katika giza, bali alikuwa daima na mwanga~~zo~~ wa uzima. (Yoh.8.12.)

Yesu alimwuliza kipofu ~~wa macho~~ akisema: "Wataka nikufanyizie nini?" Naye akasema: "Bwana, nipate kuona. " Yesu akamwambia: "Ona! Imani yako imekuponya." Mara hapo akapata kuona akamfuata Yesu.(Lc. 10,12)

Mfalme Daudi alizoea kusali: "Ee Mungu, uyaangazie macho yangu, nisianguke na kufa, adui yangu asipate kusimanga na kusema: "Nimemshinda."

Tusali mara nyingi: Maria mtakatifu, mama wa Mungu, utuombee, sasa na saa ya kufa!"

Mtakatifu Maria M a g d a l e n a, Posteli

+ 16.7.1846.

Wakati wa dhoruba.

Radi zilipigapiga kwa nguvu. Ngurumu ulisikilika daima. Mawingu meusi yalinyesha mvua kama mito. Hata wanaume hodari walitetemeka.

Palikuwa na mwanamke nyumbani mwake aliyekuwa akihangaikahangaika. Alijaribu kumshika mwana wake karibu naye. Bure! Mtoto huyu, jina lake Yulia, alikimbia dirishani mara kwa mara. Dhoruba ilizidi na mtoto alizidi kufurahi. Hata alianza kupiga makofi ya changamko.

"We mwanangu!" alisema mama, "wafanya furaha, na wengine wote wanaona hofu?"

"Ndiyo , mama, nafurahi sana kwa sababu sasa Mungu hachokozwi. Kwani sasa naona, watu wabaya wanaacha kumtukana Mungu. Laiti radi ingepiga daima na ngurumu kusikilika daima!"

Miaka mingi ikapita. Mtoto huyu Yulia akakua na kuingia utawani. Jina lake alibadili kuwa Maria Magdalena , hata alianzisha chama cha waalimu wanawake.

Siku moja radi ilipiga kwa nguvu. Kuta na misingi ya monasterio zilitikisika. Watoto wadogo wanawake walilialia kwa hofu na kulalamika. Hapo mlango ulifunguliwa. Akaja mama mkubwa akachekelea watoto akasema: "Wanangu wapenzi, mnalia sababu gani? Mbona Mungu ni Baba yetu mwema ; hatutaki wala hatutendi mabaya!"

Baadaye alienda dirishani akaifungua akainua macho juu mbinguni akisali.

Kwa mara moja umeme na ngurumu ulikomeka. Mawingu yamegawanyika. Kumekuwa kweupe.

Maria Magdalena alipata umri wa miaka 90. Alimaliza nguvu zake zote katika kumtumikia Mungu na watu. Kweli alikuwa safi na mcha Mungu kama mtoto.

Ikiwa mawingu mazito ya mvua yalikusanyika , umeme na ngurumu zilizidi --- ndipo macho yake yalingarika. Ndipo hunena kwa watawa wenzake: "Ningependa umeme na ngurumu zingekuwa daima mbinguni. Wakati wa dhoruba watu wanaogopa adhabu ya Mungu na wanaacha kumkasirisha." Sauti ya Mungu haisikilikani mbinguni tu, lakini hata moyoni.

## Mtakatifu M e n o l f i

+ 5.10.847.

**Tazama, niko mlangoni!**

Askofu Badurado aliketi kati ya mapadre na wanafunzi wake nao waliangalia sana mafundisho yake. Alisoma katika Injili ya Mateo sura 8, aya 20: "Wabweha wana matundu, na ndege za anga wana vituo, ila Mwana wa mtu hana mahali pa kulaza kichwa chake." Halafu aliwatazamia mmoja ~~kwa~~ mmoja akiuliza maana ya masomo hayo.

Basi akasimama mmoja akanena: "Kristu alitaka makao mioyoni mwetu. Alitafutatafuta, kumbe hakupata. Ubaya wetu ulimzuia kuingia kwetu."

Maelezo hayo yalimfikirisha sana mmojawapo wa wanafunzi ndiye Menolfi. Hakuweza tena kusahau kama Yesu Kristu anapiga hodi kinyenyekevu, lakini mara nyingi bure tu.

Hapo basi alikusudia kabisa: "Mimi nataka kumfungulia Mkombozi mlango wa moyo wangu. Kwa hivi hata yeye atanifungulia nitakapopiga hodi mlangoni kwa mbinguni."

Naye alishika ahadi yake kiaminifu. Alifanya moyo wake kuwa hekalu takatifu la Mungu. Alijenga monasterio ambamo wanawake watawa walipata nafasi ya "Kumpenda Kristu kuliko yote." Tena alifanya bidii kueneza dini hata wapagani wapate kusikia sauti ya Mkombozi na kumfungulia mioyo yao.

Mkombozi wetu Yesu Kristu alimfunulia Yohannes mtakatifu akinena: "Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu na kufungua mlango, nitaingia kwake, nitakula pamoja naye na yeye pamoja nami."

Mara nyingi Yesu Kristu anabisha kwako akikuita kumkaribisha katika Komunio takatifu.-

Au labda anakuita kufanya kazi yake ya kueneza dini kama padre au mwalimu au mtawa au katika aksyo katoliki - haya, itika!

## Mtakatifu F o k a s , mshahidi wa dini

Aliuawa wakati wa udhulumu mkubwa wa Wakristu. Sikukuu yake 22.Septemba.
"Mauti, uchungu wako u wapi?"

Fokas alikuwa fundi wa bustani mjini mwa Sinope, ulio mji mkubwa karibu na bahari nyeusi. Bustani moja mbele ya mji na nyumba moja ndani yake zilikuwa mali yake. Alijipatia riziki kwa kazi ya mikono yake. Lakini bidii zaidi alifanya katika kazi ya Mungu. Kwani alikuwa mkristo hodari. Wakati ule sifa hiyo ilileta hatari kubwa.

Siku moja askari walikuja kwake. Bila kujua waliomba malalo kwa yule waliomtafuta. Kwanza walificha kusudi lao. Walitaka kuuliza watu mjini: Fokas ni nani, na yu wapi? Baadaye walitaka kumrukia kama vile Wayahudi walivyomkamata Yesu, Yuda akiwa kiongozi wao.

Hawakujua kwamba mnyama amekwisha ingia katika wavu. Lakini walipokaa mezani na kuzungumza na kuchekacheka, Fokas aliwauliza : "Ninyi ni nani, na nia yenu ni nini?"

Ndipo walimdhihirishia kusudi lao wakamwomba awasaidie kumkamata mkristo huyu.

Kimya aliwasikiliza. Hakujifichua wala kwa neno wala kwa kikao chake. Hakuogopa kamwe wala kuhangaika. Hakufikiri la kutoroka.

Akajibu kwa taratibu: "Namjua mtu huyu. Tutampata. Nitamwonyesheni kesho. Sasa lakini pumzikeni katika nyumba yangu." Halafu alikwenda nje akachimba kaburi lake akaweka yote tayari yanayotakiwa kwa maziko.

Asubuhi aliwaamsha wageni wake akawaambia: "Nimeangalia kuwapatia Fokas mnayemtafuta."

Wakamwuliza kwa haraka: "Yuko wapi?"

"Yuko karibu sana. Anasimama mbele ya macho yenu. Ndimi mwenyewe Fokas. Basi fanyeni mnavyotaka."

Wao lakini walishituka kabisa. Hawakujua la kufanya. Walikawia kumwua mtu aliyewapokea nyumbani mwake kwa ukarimu na upendo.

Hatimaye ubaya wao ulishinda mawazo ya huruma. Wakamrukia Fokas wakamkata kichwa chake.

Hapo harufu ya damu yake ilipanda juu mbele ya kiti cha enzi ya Mungu.

Amri kuu ndiyo hiyo: Umpende Mungu kuliko yote yaani uwe tayari kuacha yote, hata uzima kwa ajili ya Mungu.

## Mtakatifu B a r u l a , mshahidi

+ 18.11.303.

Imani.

Bwana shauri Asklepiades aliumuka kwa hasira akisema: "Wasema nini? Dini yetu ni upuzi? Makaisari wetu wakiabudu miungu ni upuzi?"

Mshtakiwa ni mtakatifu mweremiti Romanus. Naye akajibu: "Ndiyo! Ni upuzi, na tena si kidogo! Mwite mtoto mmojawapo sokoni ukamwulize. Kila mtoto atasema hivi hivi!"

Basi mwamuzi alikubali neno hili. Akaletewa mtoto mdogo, jina lake Barula, aliyekuwa akicheza barabarani. Akaulizwa: "Sema,mwanangu, yafaa kuabudu Mungu mmoja tu au miungu iliyowekwa na watu?"

Pasipo hofu mtoto alijibu: "Lazima kumwabudu Mungu mmoja tu ndiye aliyeumba vitu vyote kwa neno lake tu. Kwa maana miungu ni vitu vilivyotengenezwa na watu wenyewe kwa mawe au miti. Hakika ni upuzi kuabudu miungu!"

Mwamuzi akaghadhibika mno akatoa amri: "Mwondosheni, mpigeni kiboko!" Askari wakafanya walivyoamriwa.

Baadaye Bwana shauri akaendelea kuuliza: "Nani aliyekufundisha maneno hayo?"

Mtoto akajibu: "Sikufundishwa na mtu ye yote. Ila kila asubuhi nilisikia mama yangu akisali: "Ee Mungu wa pekee, nawe Yesu Kristo! Neno hili nimepata kusikia kila siku kwa mama yangu naye mama alilipata kwa Mungu."

Kwa ukali mdhalimu akasema: "Basi hata wewe mkristo?"

Mtoto: "Ndiyo. Mimi mkristo. Namtumaini Yesu Kristo sawa na mamangu!" Basi mjeuri alimwita mama akamwonyesha mpenzi wake katika damu yake. Alipomwona mama yake mtoto alimwambia: "Mamangu, nipe maji! Naona kiu sana!"

Mama yule: "Mwanangu, burai maji ya duniani. Nenda kwa Yesu Kristo aliye kisima cha maji ya uzima wa milele. Yesu aliyechagua hata watoto kuwa mashahidi wake, atakuburudisha!"

Loo! Mtoto alikuwa radhi. Asubuhi yake alikatwa kichwa chake.

Hata wewe umepewa imani na mama, labda na mama mzazi, tena kabisa na Mama yule aliye juu" (Gal. 4.26) yaani kanisa takatifu katoliki. Basi penda imani yako ukaitimize kwa mwenendo wako. Na hayo unayosadiki na unayopenda, basi, uyakiri kwa uhodari mbele ya watu. Kumbuka neno hili: "Imani nimejulishwa na mama yangu, naye mama amejulishwa na Mungu!"

## Mtakatifu S e r v u l u s, maskini

+ 590, mjini mwa Roma

Wenye heri maskini!

Papa mtakatifu Gregori asimulia habari ya mtu fulani, jina lake Servulus.

"Alikuwa hana mali ya dunia, lakini alikuwa tajiri mbele ya Mungu. Alipoweza hufika kanisani kila siku. Baadaye alishikwa na ugonjwa wa miaka mingi, hata alishindwa kujipindua kitandani. Mama yake na mdogo wake walimtunza. Zaka alizopata hugawanya wengine au alinunua vitabu vitakatifu.

Kwa kuwa hakujifunza kusoma, huomba wageni aliowapokea nyumbani mwake wamsomee katika vitabu hivi. Hivyo alipata kujua yaliyomo ndani yake, ijapokuwa yeye hakujua hata herufi. Alikumbuka mateso ya Bwana wetu Yesu Kristu naye alivumilia mateso yake mengi na makubwa, hata alijizoea kumsifu Mungu mara nyingi na kujitolea mchana na usiku.

Basi ulikaribia wakati wa kupata mshahara wa uvumilivu wake. Mwenye kufahamu kama kufa kwake ku karibu, aliwasihi wageni wake wamsaidie kusali na kuimba, kumwabudu na kumshukuru Mungu.

Mara hapo walipoimba Servulus aliwanyamazisha : "Kimya! Kimya! Angalieni! Hamsikii nyimbo zitokazo mbinguni?" Aliposikiliza nyimbo za watakatifu na malaika waliofika kumchukua, roho yake iliacha mwili maskini. Mara nyumba yote ilijaa harufu nzuri mno. Kwa hivi waliohudhuria walifahamu kama roho ya maskini huyu imehamishwa mbinguni kama roho ya Lazarus maskini."

Papa Gregori alimaliza hadithi hiyo kwa kusema: "Tutasemaje tutakapomwona huyu Servulus aliyeshindwa kutumia mikono na miguu, lakini asiyeshindwa kufanya kazi ya Mungu?

Ndugu zangu, kumbukeni mara kwa mara habari ya mtakatifu Servulus! Mkifuata sasa mfano wa mtakatifu duniani, mtaweza halafu kufurahi pamoja nao mbinguni!"

"Mtu ajiwekeaye hazina ya mali, nao si tajiri kwa Mungu." Lc.12,21.

# Mtakatifu V i n z e n t i

+ 5.4. 1419.

Maji ya ajabu.

Siku moja mwanamke alifika kwa mtakatifu Vinzenti. Mwenye uchungu sana akamchongea mume wake akisema: "Huyu mume ni mtu mbaya kabisa, mkorofi na mkali sana. Siwezi tena kuvumilia. Baba,nifanyeje? Unionyeshe njia ya kurudisha amani nyumbani!"

Mtakatifu Vinzenti akamjibu: "Haya, nenda kwa Bruda yule anayelinda mlango wa monasterio yetu, akupe birika na maji aliyochota katika kisima chetu. Basi wakati mumeo atakaporudi nyumbani konga maji kidogo ya maji hayo. Lakini usiyameze! Lazima yakae midomoni. Ndipo utaona maajabu!"

Mwanamke aliahidi kufanya yote aliyoambiwa. Saa ya jioni mume yule aliporudi nyumbani mara alianza kuudhi na kutukana. Upesi sana bibi alikonga funda la maji akayafunga sana midomoni kusudi maji yasitoke.

Loo! Punde si punde mume alinyamaza. Hakika kwa leo hatari imepita.

Hata siku nyingine bibi huyu alijaribu dawa ile na kila mara aliona ajabu. Naye mume aligeuka kabisa. Alianza tena kuongea na bibi kwa upendo, hata alimsifu kwa sababu ya upole na uvumilivu wake.

Mwanamke mwenye furaha sana sana alimwendea tena mtakatifu Vinzenti akampasha habari kwamba maji yale ni dawa kweli kweli, imetenda miujiza.

Mtakatifu Vinzenti alicheka akinena: "Mwanangu, maji uliyoyapewa nami hayakutenda mwujiza, lakini kimya chako. Zamani ulimchokoza mumeo kwa ukinzani wako. Sasa basi, kimya chako kimemtuliza."

Hata siku hizi watu wa nchi ile hunena: "Konga maji ya mtakatifu Vinzenti!"

Haikosi nasi tutaona maajabu mara kwa mara tukitwaa funda la maji hayo.